

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**

HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKOZA WA MTWARA

Simu Na: 023 2410030

Nukushi: 023 2410030

Baruapepe:ded@tandahimbadc.go.tz

Tovuti.www.tandahimbadc.go.tz

Unapojibu taafadhali taja



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),

S.L.P. 03,

TANDAHIMBA.

Kumb. Na. JB.124/294/01A/95

24 May, 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba anawatangazia waombaji wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba kuleta maombi ya kazi kwa nafasi iliyoainishwa hapo chini, baada ya kupata kibali cha ajira chenye Kumb. Na .FA.97/228/01/9 cha tarehe 13 May, 2022, kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu ajira mpya. Hivyo basi Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Tandahimba anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi husika.

KATIBU MUHTASI III (NAFASI 4)

i. Sifa za Kitaaluma kwa mwombaji.

- a) Awe amehitimoo Elimu ya Kidato cha Nne au Sita.
- b) Awe amepata mafunzo ya Uhazili na kufaulu mitihani ya hatua ya tatu.

- c) Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja.
- d) Awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika Program za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

ii. **Mshahara**

Ngazi ya mshahara **TGS B** kwa mwezi, kulingana na viwango vya Serikali vy a nafasi hiyo.

iii. **Majukumu ya Katibu Muhtasi III**

- a) Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- b) Kusaidia kupokea wageni, na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- c) Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miradi, wageni tarehe za vikao, safari za wakuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anayofanya kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- d) Kusaidia kutatua na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka, au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi ofisini.
- e) Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote atakazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- f) Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa waliopo katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- g) Kutekeleza shughuli zozote atakazokuwa amepangiwa na mkuu wake wa kazi.

MASHARTI YA JUMLA YA WAOMBALI WA NAFASI YA KAZI

- a) Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania mwenye Umri kuanzia miaka 18 na wasizidi umri wa miaka 45.

- b) Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.
- c) Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- d) Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma , Kidato cha Nne na vyeti vya mafunzo mbalimbali vinavyohusika.
- e) Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yanayo jitoshaleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika, pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- f) Waombaji waambatanishe na picha ndogo 2 pasport size zilizopigwa hivi karibuni.
- g) "Testimonials" , "***provisional results***" , "***statement of results***" ,
Hati ya matokeo ya Kidato cha nne "***result slip***" havitakubaliwa.
- h) Waombaji wenye vyeti vya kidato cha Nne na Cheti cha Taaluma ambao vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundu (NACTE).
- i) Waombaji waliofukuzwa kazi, kupunguzwa au kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi.
- j) Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa tu kama wana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- k) Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili.
- l) Uwasilishaji wa taarifa za kugushi utaadhibiwa kisheria; aidha, maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili au kingereza na yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja Masjala ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba au kutumwa kuititia posta kwa anuani ifuatayo;

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P O3,
TANDAHIMBA – MTWARA.**

j) Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 06 June, 2022 saa 9:30 mchana.


 Robert E. Mwanawima
 Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W),
TANDAHIMBA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
 S.L.P. Box 03
TANDAHIMBA